

**TAARIFA FUPI YA KAMPENI YA KUPIMA VVU NA
KUANZA DAWA ZA ARV MAPEMA IJULIKANAYO KAMA
“FURAHA YANGU”
YENYE KAULI MBIU: “PIMA, JITAMBUE, ISHI”**

Utangulizi

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro inafanya uzinduzi wa Kampeni ya Kimkoa ya Upimaji wa VVU na kuanza ARV mapema ili kutekeleza agizo la **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb)** alilotoa kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kusimamia utekelezaji wa kampeni hii katika maeneo yao.

Maandalizi ya uzinduzi wa Kampeni hii yameratibiwa na kikosi kazi kilichoundwa chini ya Uwenyekiti wa Katibu Tawala Mkoa na kujumuisha wataalamu toka Sekretarieti ya Mkoa, TACAIDS, Halmashauri ya Manispaa ya Moshi pamoja na Wadau wetu wa mwitikio wa VVU na UKIMWI katika mkoa wetu wakiwemo **EGPAF, JHPIEGO, PACT/NAFGEM, THPS, TULONGE AFYA, TAWREF, na MWAMI FOUNDATION.**

Jukumu kuu la kikosi kazi baada ya uzinduzi wa Kimkoa ni kusimamia, kufuatilia na kutathimini utekelezaji wa kampeni mkoa mzima hadi tarehe 30 Novemba 2018, itakapowasilisha taarifa ya utekelezaji Taifani ili itangazwe rasmi tarehe Mosi Desemba 2018 kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani.

Madhumuni ya Kampeni

Madhumini ya kampeni hii ni kufikia malengo ya Tanzania, kwamba ifikapo mwaka 2020 asilimia 90 ya watu wanaoishi na VVU wanatambua hali zao za maambukizi, asilimia 90 kati yao waanze kutumia dawa za kufubaza VVU na asilimia 90 ya wanaotumia dawa za kufubaza VVU, kiwango chao cha VVU mwilini kiwe kimeshuka.

Malengo ya Mkoa

Kimkoa tumejiwekea malengo ya kuwafikia watu wapatao 73,605 ifikapo Novemba 30, 2018 kama ifuatavyo;

- Halmashauri ya Wilaya ya Hai – watu 4,583
- Halmashauri ya Wilaya ya Moshi – watu 21,786
- Halmashauri ya Manispaa ya Moshi – watu 13,467
- Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga – watu 4,935
- Halmashauri ya Wilaya ya Rombo – watu 6,689
- Halmashauri ya Wilaya ya Same – watu 13,175

- Halmashauri ya Wilaya ya Siha – watu 8,970

Uhamasishaji

Ili kufanikisha mwitikio wa wananchi kushiriki katika kampeni hii, njia mbalimbali za uhamasishaji zilitumika ikiwemo matangazo kwenye radio za kijamii (Fountain na Boma Hai FM), matangazo kwenye maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa watu kwa kutumia gari la matangazo, Barua kwenye taasisi mbalimbali ikiwemo Makanisani na Misikitini.

Kimkoa wiki ya Kampeni ilianza tarehe 10/9/2018 katika viwanja vya Shree Hindu Mandal na itamalizika tarehe 16/9/2018. Aidha Kampeni itazinduliwa katika Halmashauri zote ndani ya wiki moja baada ya uzinduzi wa Kimkoa. Kampeni itaendelea kwa huduma kutolewa kwa njia ya huduma mkoba na kwenye vituo vya huduma za afya hadi tarehe 30 Novemba, 2018.

Matokeo ya utekelezaji wa kampeni:

Matokeo ya siku tatu za mwanzo za wiki ya kampeni yameonyesha mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na mwitikio mzuri wa wanaume kujitokeza kupima VVU. Aidha kumekuwa na mwitikio mzuri wa wananchi kujitokeza kujitolea kuchangia damu, kupima magonjwa sugu yasiyoambukiza, kupima uwiano wa uzito na urefu na

kuhamasika kuchukua kondom kama kinga ya maambukizi ya VVU.

Mchanganua wa mafanikio kwa siku 3 za mwanzo ni kama ifuatavyo:

1. Upimaji VVU

- Jumla ya watu 1369 walipima VVU, wanaume wakiwa 905 (66%) na wanawake 464 (34%)
- Aidha watu 11 (0.8%) waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU, wanaume wakiwa 6 (0.7%) na wanawake 5 (1.1%)
- Wote wameunganishwa na huduma za Tiba na Matunzo kwa ajili ya kuanza dawa.

2. Magonjwa yasiyoambukizwa

- Jumla ya watu 499 walijitokeza kwenye huduma ya magonjwa yasiyoambukiza wanaume wakiwa 302 (61%) na wanawake 197 (39%).
- Waliogundulika kuwa na shinikizo la damu walikuwa 77 (15%) (wanaume 53 (18%) na wanawake 24) (12%)
- Jumla ya watu 22 (4%) waligundulika kuwa na sukari ya kupanda wanaume wakiwa 14 (5%) na wanawake 8 (4%)

- Aidha watu wapatao 238 waliopima uwiano wa uzito na urefu (Body Mass Index) wanaume wakiwa 102 na wanawake 136 waligundulika kuwa na hali duni ya lishe.
- **Watu wote waliogundulika kuwa na magonjwa yasiyoambukiza walipatiwa ushauri na tiba kulingana na majibu ya vipimo.**

3. Kuchangia damu

- Jumla ya watu 66 walijitokeza kuchangia damu na kufanikiwa kupata kiasi cha chupa 66 za damu.

4. Huduma ya Afya ya Uzazi

- Jumla ya watu 116 walijitokeza kwenye huduma ya afya ya uzazi wanaume wakiwa 18 na wanawake 98.
- Aidha wanawake wapatao 40 walichagua njia ya vipandikizi, 18 njia ya sindano na 18 njia ya vidonge.
- Jumla ya watu 36 walipata tu huduma ya ushauri
- Pia jumla ya kondom 24601 ziligawiwa kwa watu baada ya kupewa elimu na maelekezo ya matumizi sahihi.

5. Huduma ya macho

- Jumla ya watu 224 walijitokeza kupima macho na katimyao 138 waligundulika kuwa na matatizo ya macho na kupewa ushauri na rufaa kulingana na tatizo.

HITIMISHO

Baada ya kumaliza wiki ya kampeni huduma ya upimaji itaendele kutolewa kwenye vituo vya huduma na kwa njia ya mkoba.

Naomba kuwasilisha,

ASANTENI

